**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**PWANI – MEI, 2022**

# TAKUKURU PWANI YATAJA VIPAUMBELE VYAKE KATIKA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

**Ndugu wanahabari,**

Ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Awali ya yote na kwa namna ya pekee ninaomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuifikia siku ya leo na kutukutanisha mahali hapa tukiwa na afya njema na wenye nguvu za kuendelea kufanya kazi kwa weledi na ustadi zaidi. Nimewaalikeni kuja hapa ili kupitia kwenu, Watanzania wote wafahamu kazi zilizotekelezwa na TAKUKURU Mkoa wa Pwani kwa kipindi cha Mwezi Januari hadi Machi, 2022.

Ikumbukwe kuwa ni utaratibu wetu kufanya hivyo ili umma wa Watanzania ufahamu tunafanya nini, pia watambue vipaumbele vyetu katika mapambano dhidi ya Rushwa na hatimaye wananchi wahamasike kuunga mkono juhudi za mapambano dhidi ya Rushwa nchini. Kwa msingi huo naomba kuainisha kazi zilizotekelezwa na TAKUKURU Mkoa wa Pwani kwa mgawanyo wa maeneo makuu manne (4) yafuatayo:- Uzuiaji Rushwa; Uelimishaji Umma; Uchunguzi na huduma za Sheria pamoja na Ushirikiano na wadau katika mapambano dhidi ya Rushwa.

## UZUIAJI RUSHWA

Katika eneo la Uzuiaji Rushwa tulifanya chambuzi za mifumo katika sekta za **Elimu na Ujenzi.**

- Katika elimu tulifanya **uchambuzi wa mfumo kuhusu uchangishwaji wa michango kwa shule za msingi.** Kupitia uchambuzi huu TAKUKURU kwa kushirikiana na wadau wa elimu wa wa shule hizo tulifanya kikao kazi (Warsha) na kuweka maazimio ya kutekeleza ili kuondoa changamoto au mapungufu yanayoweza kubainika katika zoezi la ukusanyaji wa michango hiyo.

- Katika sekta ya ujenzi tulifanya uchambuzi wa mfumo wa utendaji kazi wa TEMESA na kubaini baadhi ya mapungufu madogo ambayo tayari TAKUKURU tumeshakaa na wahusika na tumeelekezana namna bora ya kutatua au kuondoa mapungufu hayo.

## UFUATILIAJI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### Ndugu waandishi wa habari,

Katika robo hii ya mwaka, tumefuatilia jumla ya miradi ya maendeleo **182** katika Sekta za Afya, Elimu, ujenzi na Maji. Miradi hiyo ina thamani ya **Shilingi Bilioni nane, milioni mia nne sabini na nane, laki tisa arobaini na moja elfu na mia tano (8,478,941,500/=).**

Miradi hiyo ilihusiana na ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na sekondari maarufu kama madarasa ya UVIKO 19, ambapo kasoro chache zilizobainika kama vile nyufa zilizojitokeza maeneo ya dirishani zilifanyiwa marekebisho na wakandarasi baada ya ufuatiliaji. Pia tulifuatilia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara za TARURA ambapo baadhi ya miradi kazi ilifanywa kidogo lakini mkandarasi alilipwa pesa yote ya kipengele kimojawapo katika mkataba, tofauti na uhalisia wa kazi iliyofanyika. Yaani kulikuwa hakuna "value for money" na pia mkandarasi aliyetelekeza mradi hakuwepo eneo la mradi bila taarifa kwa miezi mitatu. Hivyo TAKUKURU ilielekeza mkandarasi huyo arudi kazini na kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa mkataba na kazi hiyo imeshaanza kufanyika.

## UCHUNGUZI NA HUDUMA ZA SHERIA

Kwa robo hii ya mwaka, ofisi ilipokea jumla ya **malalamiko 98.** Kati ya malalamiko hayo, malalamiko **51** yalihusu Rushwa na malalamiko **47** hayakuhusu rushwa. Malalamiko **51** ambayo yaliyohusu rushwa yalianzishiwa majalada ya uchunguzi ambao bado unaendelea. Malalamiko **47** ambayo hayakuhusiana na rushwa, walalamikaji **46** walielimishwa na kushauriwa ili kutatua tatizo husika na mlalamikaji **1** taarifa yake ilihamishiwa idara nyingine.

**Mchanganuo wa takwimu za taarifa kiidara ni kama ifuatavyo:**

Afya- 4; Ardhi- 17; Mahakama- 6; Elimu- 7; Jeshi la Ulinzi-2; Maliasili na Misitu- 4; Michezo- 1; Mawasiliano- 1; Mamlaka ya Mapato- 1; Utawala-7; Nishati- 3; Siasa-1; Jeshi la polisi- 11; Tamisemi- 25; Usafirishaji- 1; Binafsi-4 na Ushirika-3.

Katika kipindi husika, kesi mpya **2** zilifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya **mashauri 17** kuendelea mahakamani. Aidha, kesi **2** zilitolewa maamuzi na mahakama zetu wilayani Mkuranga na Kibiti ambapo kesi moja tulishinda na kesi moja tulishindwa.

## ELIMU KWA UMMA.

**Ndugu waandishi wa habari,**

Katika kuhamasisha umma wa watanzania kushiriki mapambano dhidi ya rushwa nchini, elimu ilitolewa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa TAKUKURU ambapo Jumla ya **kazi 151** za uelimishaji umma zilifanyika zikiwemo **semina 13, mikutano ya hadhara 39, maonesho 2**, **vipindi vya redio na Runinga 5; taarifa 1** ilitolewa kwa **vyombo vya habari; makala 12** ziliandikwa pamoja na kuimarisha jumla ya **klabu za wapinga rushwa 79**.

Malengo mahususi ya kutoa elimu hii kwa jamii yalikuwa ni kubadili mtazamo wa wananchi kuhusiana na kuzuia na kupambana na rushwa,

kuongeza ufahamu na uelewa wa wadau juu za kampeni ya mapambano dhidi ya rushwa na kuwawezesha wananchi kuchukua hatua stahiki, kuimarisha uwezo na ufanisi wa wadau wanaoshiriki mapambano dhidi ya rushwa.

## USHIRIKI WA WADAU

TAKUKURU inatambua umuhimu wa ushiriki wa wananchi na wadau kwenye mapambano dhidi ya rushwa na kupitia programu za uelimishaji umma tumefanikiwa kuwafikia wananchi kwa njia mbali mbali ikiwemo kulifikia kundi la Vijana wa Skauti. TAKUKURU imefanikiwa kuanzisha ushirikiano na Chama cha Skauti Tanzania na kuunda ushirika uitwao TAKUSKA. Kupitia ushirikiano huu, tunatarajia kufikisha ujumbe wa mapambano dhidi ya Rushwa kwa jamii kwa kutumia vijana wa skauti ambao wameshaanza kupata mafunzo maalum ili waweze kutumika katika kuelimisha jamii hususani mashuleni na vyuoni ili jamii ya watanzania iweze kuelewa umuhimu wa kukataa Rushwa na hatimaye waweze kuunga mkono juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya Rushwa nchini.

Kutokana na ushirikishaji wa wanachi kupitia uelimishaji umma yamekuwepo matokeo chanya katika kuzuia vitendo vya rushwa na ubadhilifu nchini ambapo wananchi wamekuwa ni sehemu ya mafanikio ya vita ya rushwa na ufisadi kwa kuwafichua wanaojihusisha na vitendo hivyo, kutoa ushahidi mahakamani na kutambua wajibu wao wa kusimamia miradi ya maendeleo kwa kushirikiana na Serikali. Kama ambavyo tumeshuhudia miezi michache iliyopita jinsi jamii ilivyoshiriki vyema katika usimamizi wa miradi ya ujenzi wa madarasa ya UVIKO - 19 ambapo madarasa yamejengwa kwa ubora uliotakiwa, hayo ndio matunda ya umma kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa kwa vitendo.

TAKUKURU pia, ilishirikiana kwa ukaribu na kamati za Ulinzi na Usalama ya Mkoa na wilaya zake zote, wakiwemo wakurugenzi wa Halmashauri na wakuu wa idara na katika kuhakikisha MKAKATI WA KUWATUMIA SKAUTI KUTOA ELIMU YA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA mashuleni na vyuoni

inafanikiwa. Kamati hizi za ulinzi na usalama wamejitolea kuwa mstari wa mbele kuhakikisha mkakati huo unafanikiwa katika mkoa wetu chini ya uongozi wa Mkuu wa Mkoa ambapo tayari uzinduzi wa mkakati huo ulikwishafanyika. Na sasa ngazi ya wilaya wanaendelea na uzinduzi wa mwongozo huo ili utekelezaji uanze kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

Aidha, tuliweza kuwafikia wananchi na kusikiliza kero zao kwa utaratibu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA (PCCB MOBILE). Utaratibu huu umekuwa na mafanikio makubwa sana katika vita dhidi ya Rushwa mkoani Pwani kwani wananchi wengi wamekuwa wakijitokeza kuwasilisha kero zao na kuweza kupata ufafanuzi juu ya kero walizonazo ndani ya muda mfupi. Na kupitia utaratibu huu wananchi wamekuwa wakiunga mkono juhudi za TAKUKURU katika kupambana na Rushwa kwa kutoa ushirikiano na kujitokeza kutoa ushahidi mahakamani pindi wanapohitajika kufanya hivyo.

Elimu tuliyotoa kwa kipindi tajwa ilihusu mambo yafuatayo:-

1. **Makatazo ya Rushwa kwa mujibu wa vitabu vitakatifu vya Mungu;**
2. **Umuhimu wa wananchi kusimamia miradi ya Maendeleo**
3. Kupitia kampeni yetu ya **Vunja Ukimya: Kataa Rushwa Ya Ngono** elimu juu ya madhara ya rushwa ya ngono ilitolewa kwa jamii ikiwa na lengo la kuonyesha nafasi ya wananchi katika ushiriki wa kampeni hii na kuhamasisha umma kuwa jasiri katika kutoa taarifa za rushwa ya ngono.

**MAADHIMISHO:**

Katika kipindi hiki TAKUKURU mkoa wa Pwani ilishiriki katika shughuli mbalimbali za kitaifa ambapo Machi 8, 2022 tulishiriki kwenye MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI yaliyofanyika kimkoa huko Chalinze wilayani Bagamoyo kwa kufanya onesho kwa umma wa watanzania ambapo elimu ya Rushwa ilitolewa na kuihamasisha jamii kushiriki mapambano dhidi ya rushwa kwa vitendo.

Aidha, TAKUKURU mkoa wa Pwani ilishiriki kuadhimisha WIKI YA SHERIA kwa kuandaa semina mbalimbali kwa idara za serikali na jamii nzima ya wanaPwani kwa kutumia utaratibu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA kufikisha elimu kwa jamii ili kuhamasisha watanzania kushiriki vita dhidi ya Rushwa kwa vitendo.

## MIKAKATI YETU KWA KIPINDI CHA APRILI HADI JUNI, 2022

Kwa kipindi cha robo mwaka ya Aprili mpaka Juni, 2022 TAKUKURU mkoa wa Pwani pamoja na kazi nyingine itajikita katika kutekeleza maelekezo ya serikali na miongozo yake kwa kuongeza tija kwa vipaumbele vifuatavyo:

- **Kuzuia** vitendo vya Rushwa na ufisadi kabla havijatokea kwa kufuatilia miradi ya maendelea kwa hatua zote ili kuhakikisha rasilimali fedha za watanzania zinatumika pasipo kuhujumiwa au kufanyiwa ubadhirifu wa aina yoyote.
- Kuendelea **kuelimisha** umma wa watanzania juu ya madhara ya rushwa ili wafahamu nafasi yao katika mapambano dhidi ya rushwa kwani vita hii si ya TAKUKURU peke yake bali ni ya watanzania wote.
- Aidha, kwakuwa tunaelekea kwenye chaguzi za ndani za vyama vya siasa ni dhamira ya TAKUKURU mkoa wa Pwani kufuatilia chaguzi hizi, hatutakaa nyuma bali tutajikita katika kutoa elimu juu ya madhara ya Rushwa katika chaguzi za kisiasa ili umma uweze kuchagua viongozi safi wasio na mawaa au harufu ya Rushwa.
- Kuendelea kufanya ufuatiliaji na chambuzi za mifumo kwa lengo la kuziba mianya ya rushwa itakayobainika, kwani ni imani yetu kwamba rushwa itakoma kwa kudhibitiwa kabla haijatendeka hivyo ni vyema kufanya uchambuzi wa mifumo na kuweka mikakati thabiti ya kuziba mianya iliyomo ndani ya mifumo hiyo ya utendaji.
- Kuendelea kukagua utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo katika mkoa wetu ili miradi hiyo iweze kutekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa na kwa ubora unaostahili na kuleta tija kwa jamii.

## WITO WA TAKUKURU KWA WANANCHI

**Ndugu waandishi na wananchi,**

Naomba kutumia fursa hii kuwasihi wananchi wa mkoa wa Pwani kufanya kazi kwa uadilifu kwa kuepuka vitendo vya Rushwa kwani chini ya utawala ya Rais wetu mpendwa MAMA SAMIA SULUHU HASSAN na kwa uimara wa TAKUKURU hawatabaki salama. Sote tunafahamu kuwa Rushwa ni adui namba moja wa maendeleo ya nchi yetu, na kwakuwa dhamira ya Serikali yetu ni kuleta maendeleo basi hatuna budi kuepukana na vitendo vya Rushwa.

Aidha, kama mnavyofahamu tunaelekea kwenye harakati za uchaguzi wa ndani wa baadhi ya vyama, niwaombe sana tutumie fursa tuliyonayo kuchagua viongozi waadilifu na wenye nia ya kweli ya kutatua changamoto zinazowakabili katika jamii.

Aidha, niwasihi sana watanzania wenzangu tuendelee kusimamia miradi ya maendeleo kwa kutanguliza **uzalendo,** tuwe **waaminifu** na **waadilifu** ili kujenga Tanzania imara kadiri ya maelekezo ya serikali yetu pendwa.

**Ndugu WanaHabari,**

Mwisho, nitoe ONYO kwa wote wenye nia mbaya ya kuihujumu serikali kwenye miradi ya maendeleo. Nadhani mmeshuhudia maafisa wa TAKUKURU wakipita kukagua miradi hiyo kila wakati. Tutakuwa wakali sana kwa watu wanaojihusisha na Rushwa au ufisadi kwenye miradi hiyo ya maendeleo. Tuungane pamoja kuijenga Tanzania yenye maendeleo ya kweli kupitia miradi hii inayoanzishwa na serikali yetu.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

***Imetolewa Na:***

**CHRISTOPHER MYAVA,**

**Mkuu wa TAKUKURU (M), PWANI.**
**0738 150176**